**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE**

# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 22. 11.2021

Novemba , 2021

**AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA UKAGUZI WILAYA CHA TAREHE 24/11/2021.**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUPITISHA AGENDA
3. KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 20.09.2021
4. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 20.09.2021
5. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI OKTOBA 2021
6. UANZISHAWAJI WA SOKO LA KILELEMA NA STENDI YA GARI KUBWA (LORI)
7. MAPENDEKEZO YA VIWANGO VYA GHARAMA ZA VIBALI VYA UJENZI
8. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SEQUIP
9. MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO
10. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI
11. KUFUNGA KIKAO

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 24/11/2021

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 1.11.2021. KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 05:15 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 2.11.2021. KUPITISHA AGENDA**

Jumla ya agenda kumi na moja zilisomwa na kupitishwa na wajumbe ili ziweze kujadiliwa.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 3.11.2021. KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 20/09/2021.**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kurasa kwa kurasa kwenye muhtasari wa kikao cha tarehe 20/09/2021, na baada ya kuupitia waliruhusu usainiwe ili kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 4.11.2021. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 20/09/2021.**

Kuhusu kubadilisha matumizi ya fedha za mradi wa vijana kutoka ufyatuaji wa tofali kwenda kwenye viwanda vya useremala, iliagizwa kamati kutembelea vikundi kabla ya kupewa fedha hizo.

Agizo lilizingatiwa, ziara hiyo ilifanyika tarehe 24/11/2021 katika vikundi vya useremala vya Upendo kilichopo Buhigwe na Professional Furnitures Designers cha Kibande pamoja na kikundi cha upandaji miti cha Jiwezeshe kilichopo Buhigwe.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kuridhia na kuipitisha.

Kuhusu watumishi waliothibitishwa kazini na katika vyeo vyako vipya, iliagizwa watumishi hao, wahudhurie kikao hiki ili wajumbe waweze kuwaona.

Agizo lilizingatiwa, kwa mujibu wa kanuni, watumishi wanathibishwa na mwajiri kupitia bodi ya ajira, hivyo kamati hii ni kupewa taarifa tu, hata hivyo kumwita mtumishi ni gharama kwani wengine wanatoka mbali na Makao makuu ya Halmashauri.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuipitisha.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 5.11.2021. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI OKTOBA, 2021.**

Menejimenti iliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Oktoba, 2021 kuwa kiasi cha Tsh. 1,774,881,423.03 sawa na 69.60% ya Tsh. 2,549,936,586.28 kwa Mwezi toka vyanzo vyote vya ndani. Kwa Miezi Minne (Julai-Oktoba 2021) kiasi kilichopatikana ni Tsh. 7,569,185,142.33 sawa na 24.74 % ya lengo la Tsh. 30,599,239,035.38 kwa Mwaka.

Aidha mapato yaliyopatikana kutoka vyanzo vya ndani pekee ni Tsh. 76,063,790.49 sawa na 109.34% ya lengo la Tsh. 69,567,166.67 kwa Mwezi, na kufanya jumla ya mapato ya ndani kwa miezi Minne (Julai -Septemba 2021) kuwa Tsh. 301,834,840.98 sawa na 36.16% ya Tsh. 834,806,000.00 kwa Mwaka.

Matumizi kwa Mwezi Oktoba ni Tsh. 2,191,307,299.00 kwa Mishahara na uendeshaji wa miradi ya maendeleo na kufanya Jumla ya Matumizi kwa Miezi Minne (Julai-Septemba 2021) kuwa Tsh. 6,861,216,074.90 sawa na 22.42% ya lengo la Tsh. 30,599,239,035.38 kwa Mwaka.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuipitisha.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 6.11.2021. UANZISHWAJI WA SOKO LA KILELEMA NA STENDI YA MAGARI MAKUBWA (LORI) MUHARURO.**

Menejimenti iliwasilisha taarifa mpango wa ujenzi wa soko la mazao Kilelema na Stendi ya gari Kubwa Muharuro kama ifuatavyo;

Kwa upande wa soko ilielezwa kuwa eneo linalopendekezwa lina ukubwa wa ekari 11.5 mali ya Serikali ya Kijiji cha Kilelema lenye sifa zifuatazo, halina mazao ya kudumu, halina makazi ya watu, litajengwa daraja la mto Malagarasi na lina pitisha watu wengi kwenda Burudndi na kurudi. Aidha yalitolewa maoni kuwa,

1. Halmashauri ijenge uzio wa muda ili shughuli za biashara zianze mara moja na
2. kushirikisha wananchi katika hatua za awali za ujenzi.

Aidha kuhusu eneo la stendi ilielezwa kuwa lipo katika Msitu wa Halmashauri Muharuro na lina ukubwa wa ekari 5 na miti aina ya Mkaratusi.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuamua kamati ikatembelee maeneo hayo ili kujiridhisha kabla ya kuuanza utekelezaji.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 7.11.2021. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SEQUIP**

Menejimenti iliwasilisha taarifa ya ujenzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana Kasumo na Shule ya Kata ya Mugera katika Kijiji cha Katundu inayotekelezwa chini ya Mpango wa SEQUIP kwa muda wa miaka mitano, lengo kubwa ni kuboresha elimu kwa Watoto wakike/wasichana.

Sekondari ya Mugera itakuwa ni miongoni wa Sekondari maalum zinazojengwa Tanzania nzima na zitakuwa na majengo 56 kwa kila shule, ambapo kila shule itakuwa na jumla wanafunzi ni 1200.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuipitisha.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 8.11.2021. VIBALI VYA UJEZI.**

Menejimenti iliwasilisha mapendekezo ya bei za vibali vya ujenzi wa majengo tofauti ambayo ni tofauti na ile ya awali kama ifuatavyo;

| NA | AINA YA JENGO | BEI YA AWALI | BEI YA SASA |
|---|---|---|---|
| 1 | Jengo la Makazi lenye sakafu ya chini pekee | 10,000/= | 30,000/= |
| 2 | Jengo la makazi lenye Sakafu za juu zaidi ya 1-2 | 20,000/= | 200,000/= |
| 3 | Jengo la makazi lenyeSakafu za juu Zaidi ya 2 | 50,000/= | 300,000/= |
| 4 | Jengo la biashara lenye sakafu ya chini pekee | 10,000/= | 50,000/= |
| 5 | Jengo la biashara lenye Sakafu za juu zaidi 1-2 | 25,000/= | 200,000/= |
| 6 | Jengo la biashara lenye sakafu za juu Zaidi ya 2 | 70,000/= | 400,000/= |
| 7 | Jengo la karakana/ kiwanda | 250,000/= | 400,000/= |
| 8 | Ujenzi wa minara | 1,000,000/= | 1,000,000/= |
| 9 | Majengo matano ya chini | --- | 500,000/= |
| 10 | Jengo linalofanyiwa ukarabati tofauti na ramani ya awali | 50% ya ada ya awali | 50% ya ada ya awali |
| 11 | Jengo linalofanyiwa upanuzi | 50% ya ada ya awali | 50% ya ada ya awali |
| 12 | Jengo linalofanyiwa upanuzi na ukarabati kwa pamoja | 100% ya ada ya awali | 100% ya ada ya awali |

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuipitisha.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 9.11.2021. MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO.**

Menejimenti iliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha Tsh. 1,910,000,000.00 kwa Mchanganuo ufuatao;

1. Fedha za UVIKO zitatumika kutekelezamiradi ifuatayo,
   - Vyumba 53 vya madarasa ya sekondari Tsh. 1,060,000,000.00
   - Vyumba 2 shule shikizi Tsh. 40,000,000.00
   - Ununuzi wa X-RAY Tsh. 420,000,000.00
   - Nymba za watumishi Hospitali ya Wilaya Tsh. 90,000,000.00 na
   - Jengo la dharura Hospitali ya Wilaya Tsh. 300,000,000.00
2. Kupitia tozo ya Miamala.
   - Bweni la Wanafunzi wenye mahitaji maalum Tsh. 80,000,000.00
   - Ujenzi wa vyumba vya madarasa 15 shule za sekondari Tsh. 187,500,000/=
3. Vyanzo vingine.
   - Ujenzi wa vyoo na miundombinu ya maji katika vituo vya kutolea huduma 12 Tsh. 698,158,000.00
   - Uimarishaji wa huduma ya uhai na ulinzi wa mama na mtoto Tsh. 7,881,150

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuagiza kamati ikatembelee miradi ya awali ya vyoo na miundombinu ya maji kwa kuwa ni ya muda mrefu na haikamiliki.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 10.11.2021. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKIYI.**

Hapakuwa na mengineyo mezani kwa mwenyekiti.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 11.11.2021. KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 9:30 alasiri akiwashukuru wajumbe na wataalam kuhudhuria kikao. Aidha alisema kuwa kila mtu atomize wajibu wake kwa manufaa na maendeleo ya Halmashauri.

**MUHTASARI HUU WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 24/11/2021 UMESAINIWA NA;**

| | |
|---|---|
| JINA KAMILI: ESSAU H. NGOLOKA | JINA KAMILI: Venance Kigwinya |
| SAINI: [signature] | SAINI: [signature] |
| TAREHE: 22/12/2021 | TAREHE: 22/12/2021 |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE | MWENYEKITI HALMASHARI YA WILAYA S.L.P 443.BUHIGWE |

## MAHUDHURIO YA KIKAO CHA ~~CMT~~ FUM TAREHE 22.11.2021

| NA. | JINA KAMILI | CHEO | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Essau H. Ngoloka | Mkurugenzi Mtendaji (W) | 2:00 |
| 2 | Christian Makupa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi(W) | 2:00 |
| 3 | Nice Msuya | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (W) | 2:00 |
| 4 | Christopher Kajange | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (W) | 2:00 |
| 5 | Masau Koligo | Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira (W) | 2:00 |
| 6 | Jerry Mwakapemba | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (W) | 2:00 |
| 7 | Mussa Ilanda | Kaimu Mkuu wa idara ya Ardhi na Maliasili (W) | 2:00 |
| 8 | Weisy Y. Wikedzi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) | 2:00 |
| 9 | Charles Mabuga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi (W) | 2:00 |
| 10 | Alphonce Haule | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi (W) | 2:00 |
| 11 | Erasto Andrew | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) | 2:00 |
| 12 | Edgar Mnyavanu | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) | 2:00 |
| 13 | Dkt.T. Kamugishga | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi (W) | 2:00 |
| 14 | Dkt. Julius Nyasongo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 2:00 |
| 15 | CPA. Suphian Juma | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | 2:00 |
| 16 | Khalfan Bwangalo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria | 2:00 |
| 17 | Jacksoni Silas | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA | 2:00 |
| 18 | Mbehoma, M.C | Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari | |

### SEKRETARIET

| NA. | JINA KAMILI | CHEO | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | Pactino Kamwagila | CC | 2:00 |